JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI**

**Dar es Salaam, Jumatano Aprili 01, 2020**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inathibitisha kuwepo kwa kesi mpya ya maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) nchini iliyopatikana jijini Dar es Salaam. Mgonjwa huyu ni raia wa Marekani, Mwanamke mwenye umri wa miaka 42 ambaye amekuwa karibu na mtu aliyesafiri nje ya nchi na baadae kuthibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya COVID-19 aliporejea hapa nchini.

Hivyo hadi sasa jumla ya kesi za maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) zilizothibitishwa hapa nchini ni **ishirini (20),** ambapo wagonjwa **kumi na saba (17)** wanaendelea na matibabu na hali zao ni nzuri.

Aidha, ninatoa taarifa kuwa tarehe 31 Machi 2020 mmoja kati ya wagonjwa waliokuwa katika kituo cha matibabu cha Temeke Dar es Salaam amethibitika kupona maambukizi aliyokuwa nayo, na ameruhusiwa kurudi nyumbani na hivyo sasa kufanya jumla ya watu waliopona kuwa **wawili (2).**

**Ummy A. Mwalimu (Mb)**
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,**
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**